# MTIHANI WA PAMOJA WA KASSU

## Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari

**102/2** **KISWAHILI** **Karatasi ya 2**

**LUGHA**

**SEPTEMBA 2021 Muda: Saa $2^1/_2$**

**Jina.................................................................... Namba ya Usajili................................Darasa................**

**Tarehe .............................................Sahihi ya Mtahiniwa...................................**

***Maagizo:***

*i) Andika jina lako, nambari yako ya usajili na darasa katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*ii) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
*iii) Jibu maswali yote.*
*iv) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
*v) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
*vi) Karatasi hii ina kurasa 10 zilizopigwa chapa.*
*vii) Hakikisha kuwa kurasa zote zimepigwa chapa.*

**Kwa Matumizi Ya Mtahini Pekee**

| Swali | Upeo | Tuzo |
|---|---|---|
| 1. Ufahamu | 15 | |
| 2. Ufupisho | 15 | |
| 3. Matumizi ya Lugha | 40 | |
| 4. Isimujamii | 10 | |
| Jumla | 80 | |

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

**ULEVI**

Ilikuwa Jumamosi ya mwisho wa mwezi, wakati wa magharibi, nikiwa kwenye tembeatembea zangu za kupunga hewa. Nikaona kilee, kijitu si kijitu, mtu si mtu. Kinakuja kwa kuyumba huku na huku kama kwamba kikiendeshwa na upepo.

Kukaribiana nacho, nikaweza kukiona vizuri zaidi. Kilikuwa kirefu, lakini kilichokonda na kukondeana mithili ya kiuno cha nyigu. Shati kiliyovaa ilionekana kama kwamba imetundikwa tu kijitini. Kukikazia macho, nilitambua. Maskini! Mwili wake ulidhoofika na kuwa kitu kama vile mfuko tu wa mifupa.Kufumba na kufumbua, kilianguka bwup! Chini. Nikajikuta nakitikisa kichwa.

"Vipi Mlachake bwana we?" Nikamtupia, huku nikijaribu kumsaidia ainuke.

"Vi-vi-vipi ni-nini?" Akanirudia.

"Umerudia he?"

" La-lakini kwa pe-pesa zangu, si-si-siyo kwa-kwa-kwa kudoea."

"Daktari alikushauri vipi?

"A-ach-ch-chana naye yeye hu-huyo. Ati nina-naji-jipunguzia maisha.Kwa ni-ni-nani ha-hata-ta-kufa?"

Kuzidi kumyanyua ili nimwinue kutoka chini, akatitazama kwa macho yake malegevu na kuniuliza, "Ha-hata wewe pia una-na-nataka kuniibia?"

"Nani amekuibia?" Nikamwuliza kwa mshangao. Kimya. Aliweza kuinuka na kubaki akiyumbayumba mfano wa mcheza rumba. Kisha yakamtoka matusi mfululizo.

"Mlachake!" Ikanitoka sauti ya mshangao baada ya kushuhudia yale niliyoyatia machoni.

"Ni aibu gani hii ya kujitapikia ovyo?"

"Ni me-jiji-jitapikia ni-ndiyo. Sikumta-tapikia mtu."

"Sikiza Mlachake bwana."

"Ndi-ndiyo bwana m-mkubwa," akasema na kunipigia saluti. Kisha, kwa mara nyingine tena, huyoo akasalimu amri.

"Mlachake! Pesa, ulizifanyia, kazi mwezi mzima ili zije kukutesa namna hii he?"

"Ndi-ndiyo. Cha m-m-mgema hu-uliwa na mle-levi si-si ndiyo?"

Kwa mara nyingine tena, nilijikuta natikisa kichwa. Papo hapo, akili ikanipa kuwa nimsaidie kwa kumfikisha nyumbani kwake.

Kufika mlangoni tu, alipaaza sauti akisema, "Fungua!" Ilhali mlango ulikuwa umekomewa kutoka nje. Kisha dwa!Akaupiga teke, halafu "Huuwi!" akapiga nduru huku akishika mguu na

kutandwa na wingu jeusi usoni. “Nita-ta-charaza mtu le-le leo mimi,” akatisha. Akichutama na kubwagizika chini mfano wa gunia tupu. Nikatikisa kichwa na kujiendea zangu.

**Maswali**

a) Taja sababu mbili za Mlachake kuonekana akiyumbayumba. (Al 2)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

b) Mbali na kumletea mtu aibu kama vile ya kujitapikia ovyo, taja athari au hasara nyingine tatu za ulevi kwa mlevi (Al 3)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

c) Mwandishi anasema, “Kwa mara nyingine tena huyoo, akasalimu amri.” Anamaanisha nini hasa kwa kusema “akasalimu amri?” (Al 1)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

d) Ni aina gani mbili za ushihidi zinazotudokezea kuwa Mlachake hakuishi pekee nyumbani kwake? (Al 2)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

e) i) Ni methali gani iliyomjia Mlachake kichwani wakati alipozungumza na msimulizi wa makala hii? (Al 1)

..........................................................................................................................................

ii) Eleza jinsi methali hiyo inavyoingiliana na maudhui ya makala hii. (Al 2)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

f) Eleza matumizi yafuatayo ya lugha kama yanavyojitokeza katika makala uliyosoma. (Al 4)

i) Wakati wa magharibi

..........................................................................................................................

ii) Kukutesa

..........................................................................................................................

iii) Kudoea

......................................................................................................................................

iv) Akili ikanipa

......................................................................................................................................

2. **UFUPISHO (ALAMA 15)**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Tangu kuripotiwa kwa maambukizi na vifo kutokana na Tandavu la Korona nchini Kenya, Wakenya wengi wamekuwa wakiishi kwa hofu. Vifo vinavyohusishwa na ugonjwa huu hatari vimekuwa vikiongezeka kila kukicha. Ugonjwa huu sugu unawafisha watu kwa muda mfupi baada ya kuambukizwa. Kutokuwepo kwa dawa za kutibu ugonjwa wenyewe kunaongeza wasiwasi miongoni mwa wanajamii. Nchi ya Kenya kama ilivyo mataifa mengine ulimwenguni imehimiza raia wake kupata chanjo dhidi ya tandavu hili. Hata hivyo, hatua ya serikali kutumia vitisho ili kuwashinikiza watumishi wa umma kupata chanjo ya korona haifai kwani huenda ikatatiza mpango wa kuchanja watu milioni kumi mwaka huu. Licha ya serikali kujaribu kuwalazimisha watumishi wa umma bado chanjo haijakubalika na wengi nchini. Kutokubaliwa kwa chanjo hii kumesababishwa na ukosefu wa elimu ya kutosha kuihusu. Watu wengi wanahofia kuwa huenda waliochanjwa wakapata madhara baadaye.

Mamilioni ya watu wameathiriwa kwa njia moja au nyingine na ugonjwa huu. Kenya imeshuhudia hoteli nyingi za kifahari kufungwa. Hii imetokana na usafiri wa ndege kusitishwa kote duniani. Kutokana na hali hiyo, hoteli zilizotegemea wateja watalii zilisimamisha shughuli zake kwa muda. Kwa mfano, ya *Intercontinental* ilifunga milango yake kabisa mwaka wa 2020. Jambo hili liliwafanya watu wengi kupoteza ajira.

Usafiri wa umma umekumbwa na changamoto si haba kutokana na tandavu la korona. Serikali ilipunguza wasafiri katika magari ya abiria kwa thuluthi moja. Wasafiri hao walilazimika kulipa nauli maradufu kwa safari ile ile. Watu wengi walilazimika kufutilia mbali mipango yao ya usafiri. Kafyu vile vile iliathiri usafiri huu wa umma. Magari mengi yalilazimika kusitisha safari njiani kwa kupatikana na kafyu. Wafanyabiashara katika sekta ya matatu wanahesabu hasara kubwa kwa kukosa abiria. Wengine wamelazimika kuuza magari yao kwa kutamaushwa na changamoto iliyowakumba ghafla.

Aidha, shule zililazimika kufungwa mnamo Machi 2020. Wanafunzi walikaa nyumbani hadi Januari 2021. Hii iliharibu kalenda ya masomo nchini. Serikali ilijaribu kuwasihi walimu kufunza mtandaoni lakini hii haikufaulu hata. Wanafunzi wa kike kadhaa waliishia kupata ujauzito hivyo basi kukatiza masomo yao. Ibada zote pia zilisitishwa. Nao waumini hawakusazwa. Baada ya serikali kufunga makanisa, misikiti na vyumba vingine vya ibada,

waumini wengi walilazimika kufuatilia ibada zao katika runinga au mtandaoni. Waliokosa mitandao waliomba na jamaa zao na wengine kupuuza ibada hizo kwa muda.

Shida zilizindikana ugonjwa wenyewe ulipozidi kuenea. Hospitali za umma zililemewa na idadi ya wagonjwa waliokuwa wakienda kule kutafuta matibabu. Vitanda vilijaa na hata wengine wakalala chini katika wadi mbalimbali. Huduma za afya zikazidi kudidimia kutokana na ukosefu wa wahudumu wa afya na vifaa vya kutumiwa na wagonjwa. Vifo vingi vikaripotiwa katika hospitali hizi za umma. Kila sehemu nchini ikaathirika. Majonzi yakajaa kila mahali.
Licha ya haya mabaya yote yaliyokuja na ugonjwa huu wa corona, kuna wale waliochuma riziki kwa kuzuka kwa ugonjwa huu. Mambo mapya yalijitokeza katika ulimwengu wetu. Msamiati wa lugha ukaongezeka. Hii ilitokana na haja ya kuwepo kwa istilahi au misamiati ya kufafanua hali mpya iliyoibuliwa na tandavu hili. Vilevile Kutokana na watu kulazimika kufanya kazi nyumbani, ujuzi wa matumizi ya mtandao umeimarika. Kwa mfano, ufundishaji mtandaoni umefaidi vyuo vingi vinavyofundisha masomo ya mbali.

Wanabiashara wengine wakaanza kuuza barakoa. Barakoa ilikuwa kitu kigeni huku kwetu na duniani kwa jumla. Wengi walipata faida kubwa sana kwa kuwa soko la barakoa lilikuwa pana. Hata hivyo, barakoa zinazotumika na wananchi wengi hazijathibitishwa kuwa bora kuzuia korona. Hali hiyo inawafanya watumiaji wake kuwa na usalama wa bandia kwani wanaweza kuambukizwa ugonjwa wa korona kwa urahisi licha ya kuwa wamevalia barakoa hizo.

Kadhalika, viyeyushi vikaanza kutumika kwa wingi humu nchini na duniani kote. Wachuuzi wengi waliingia biashara hii na kufaidika kiasi. Wengi hawakujua viyeyushi ni nini kabla ya wakati huo. Hivi sasa hata watoto wadogo wanajua viyeyushi na kutumia kwa njia mwafaka.

Kundi lingine lililonawiri kwa korona ni hospitali za kibinafsi. Wengi wa matajiri walioambukizwa ugonjwa huu walijipeleka hospitali hizi kwa matibabu. Wenye hospitali hizo nao wakapandisha bei ya matibabu kwao. Ikawa ni biashara inayonoga kabisa. Hawakujali kuhusu wale wasio na pesa.

Korona imefanikisha juhudi za maafisa wa afya kuhimiza usafi kila mara. Hii ni kwa sababu watu wanalazimika kunawa mikono yao kila mara. Usafi huu wa mikono unapunguza visa vya magonjwa kama vile kipindupindu katika jamii. Aidha, gharama za sherehe zimepungua mno kutokana na sheria za kudhibiti idadi ya watu wanaohudhuria sherehe za mazishi au matanga. Hali hii ni nafuu kwa wale wachochole ambao wakati mwingine hulazimika kuuza kidogo walicho nacho ili kugharamia sherehe za matanga au arusi.

**Maswali**

a) Kwa kuzingatia aya tano za kwanza, eleza shida zilizoletwa na korona. (Maneno 100) (Al 9)

Matayarisho

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

jibu

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

b) Fupisha aya nne za mwisho kwa maneno 60. (Al 6)

Matayarisho

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

Jibu

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

.....................................................................................................................................................

.....................................................................................................................................................

.....................................................................................................................................................

.....................................................................................................................................................

**3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

a) Andika neno lenye muundo ufuatao wa sauti: (Al 2)

Kipua cha kaakaa laini, irabu ya kati tandazwa, kipasuo sighuna cha ufizi, irabu ya chini tandazwa

.....................................................................................................................................................

b) Eleza maana ya silabi. (Al 1)

.....................................................................................................................................................

c) Tambua muundo wa silabi katika neno MAKTABA. (Al 1)

.....................................................................................................................................................

d) Ainisha vipengele vilivyopigiwa mstari: (Al 2)

i) Genge <u>la</u> wezi limetiwa mbaroni.....................................................................

ii) Genge <u>la wezi</u> limetiwa mbaroni.....................................................................

e) Tunga sentensi moja ukitumia neno hili ili litumike ulivyoelekezwa mabanoni. (Al 2)

Enzi (nomino na kitenzi)

.....................................................................................................................................................

f) Eleza maana mbili ya sentensi hii: (Al 2)

Watu wa pwani hawaogopi bahari kama watu wa bara.

.....................................................................................................................................................

.....................................................................................................................................................

g) Taja matumizi matatu ya kiambishi ‘i’ na utolee mifano: (Al 3)

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

h) Ainisha mofimu za neno: Kitandani (Al 3)

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

i) Tunga sentensi moja ukitumia wakati ujao hali ya kuendelea. (Al 2)

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

j) Katika sentensi moja, tumia **papa** na **bapa** ili kudhihirisha maana ya kila neno. (Al 2)

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

k) Changanua kwa vishale: Wale wageni wetu watakuwa wamewasili leo jioni. (Al 4)

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

l) Amrisha katika nafsi ya pili wingi: **La**....................................................... (Al 2)

m) Yakinisha katika umoja: Msingalisoma nyakati zile msingalipata zawadi kemkem. (Al 1)

...........................................................................................................................

...........................................................................................................................

n) Tambua kauli iliyotumika: Ametwikwa jukumu la kuwalea yatima wale. (Al 1)

...........................................................................................................................

o) Bainisha yambwa na chagizo katika sentensi inayofuata. (Al 2)

Vibarua wamefanya kazi hiyo haraka ipasavyo.

...........................................................................................................................

p) Akifisha: (Al 2)

i) Hako katoto kalipoletwa kila mtu alikahurumia

..........................................................................................................................................

ii) Jama ni kweli umemkosea mzazi wako heshima?

..........................................................................................................................................

q) Andika katika usemi wa taarifa. (Al 3)

"Ninataka kuanza kupendekeza majina ya watakaosafiri sasa", Afisa alisema.

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

r) Vishazi tegemezi vina uamilifu gani? Taja kwa hoja mbili na utungie sentensi. (Al 2)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

s) Andika kisawe cha: enda arijojo (Al 1)

..........................................................................................................................................

t) Andika kinyume: Ajitahidiye husifiwa kwa bidii yake na hupandishwa madaraka. (Al 2)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

**4. ISIMUJAMII (ALAMA 10)**

a) Eleza majukumu matano ya Kiswahili kama lugha ya kitaifa (Al 5)

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

b) Eleza changamoto tano zinazokabili lugha ya Kiswahili kama somo katika shule za upili nchini Kenya (Al 5)

............................................................................................................................................

............................................................................................................................................

............................................................................................................................................

............................................................................................................................................

............................................................................................................................................

............................................................................................................................................

............................................................................................................................................

............................................................................................................................................

............................................................................................................................................

............................................................................................................................................

............................................................................................................................................

............................................................................................................................................